



KUTAYARISHA MBOLEA YA MBOJI KATIKA NCHI ZA HARI II



HDRA – Kwa huduma za Kilimo - hai

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Je kuna umuhimu wowote kutengeneza mboji?

Mboji haigharimu kiasi kikubwa cha pesa na huimarisha rutuba ya udongo. Viungo vya kila aina kama vile matawi, matunda na mboga, halikadhalika samadi hutumiwa katika kutayarisha mboji.

Kitabu hiki kinatoa maelezo kuhusu kutayarisha mboji katika nchi za hari. Aina ya mrundiko wa takataka ni maarufu katika kutayarisha mboji. Makala haya yanatoa maelezo kuhusu aina mbalimbali ya mifumo inayoweza kutumiwa. Aidha, kuna maelezo ya kutayarisha mboji katika sehemu zisizotumika kwa kikamilifu au zile za ukame.

Yafuatayo ni maelezo kuhusu jinsi ya kutayarisha mboji ukizingatia mitindo ya kila aina. Kwa wakulima wasio na ujuzi kuhusu mboji, ni bora kukitazama kitabu cha kwanza kisha kufuatisha hiki.

- Mboji huhitaji mchanganyiko wa viungo vilivyo na uwezo wa kuoza kwa haraka (matunda, mboga na majani ya miti) kwa pamoja na viungo vinavyochukua muda mrefu kuoza (Mabaki ya mimea na maganda). Hili ni hakikisho la muundo imara wa mboji.
- Vijidudu na vimelea ndio husababisha mboji kuoza. Viumbe hawa huhitaji mazingira muafaka ili kutekeleza jukumu hili. Kwa mfano hewa na unyevunyevu. Iwapo ni wakati wa kiangazi basi mboji yapaswa kunyunyiziwa maji.
- Sehemu za mboji hupata joto. Viwango vya joto na unyevu vyapaswa kuangaliwa, waweza kutumia kijiti katika kukadiria viwango hivi. Chovya kijiti kwenye mboji na kuwacha kwa muda fulani kisha kugusa kwa mkono. Kijiti hicho kitakuwa baridi au na joto. Iwapo hakuna dalili ya ubaridi au joto basi mboji halitafanyizwa, hivyo basi utahitajika kunyunyiza maji au kupindua.

Mboji isiyotunzwa

Kwa kawaida viungo vinavyoweza kutayarisha mboji huachwa mahali pasipo utunzi. Masalio kutoka jikoni na uchafu wa kufagiliwa hurundikwa mahali pasipotunzwa. Mahali kama hapo sio muafaka katika kutayarisha mboji kwani huchukua muda mrefu.

Mboji iliyotunzwa

Maelezo katika kitabu hiki yanafafanua jinsi ya kuimarisha na kutayarisha mboji kwa wepesi. Iwapo sehemu imetunzwa vyema, mboji hufanyizwa kwa haraka. Njia zifuatazo zimetumiwa:

- Mfumo wa Indore
- Mfumo wa Bangalore
- Mfumo wa Hamaki/Ayari
- Mfumo wa joto jingi kutoka China
- Mboji ya shimo
- Mboji ya mtaro
- Mboji ya kikapu
- Mboji ya boma
- Kutayarisha mboji kwa kutumia mabaki ya nyumbani, gugu-maji, machujo ya kahawa na samadi au kinyesi.

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Mfumo wa Indore

Mfumo huu hujumuisha tabaka zilizo na aina mbalimbali ya viungo vya kutengeneza mboji. Tayarisha sehemu ya chini yenye upana wa mita moja na urefu wa mita tatu, tumia vijiti visivyooza kwa urahisi. Mfumo huu huwezesha hewa kusambaa kwa urahisi na kuvutia vijidudu wanaosaidia katika kuoza. tabaka zitaandaliwa kama ifuatavyo:

1. Sentimita 10 ya viungo visivyooza kwa urahisi kama mabaki ya mahindi. Kisha nyunyiza maji.
2. Sentimita 10 ya viungo vinavyoweza kuoza kwa urahisi kwa mfano matunda na mabaki ya mboga.
3. Sentimita mbili ya samadi (iwapo itapatikana).
4. Kiasi kidogo cha udongo wa juu ili kutoa vijidudu na vimelea watakaosaidia katika kuoza.
5. Rudia utaratibu huu hadi kufikia kimo cha urefu wa mita moja hadi moja na nusu juu.
6. Funika kwa nyasi au majani (kama yale ya migomba) ili kuzuia kupotea kwa unyevu.

Tekeleza kazi hii kwa muda usiozidi wiki moja. Baada ya wiki 2 hadi 3 utahitajika kupindua tabaka hizo na kutayarisha upya. Hii ni kwa sababu viungo huoza kwa wakati tofauti. **Vile viungo vilivyo juu ambavyo havijaoza, vyapaswa kuwekwa kwenye tabaka la katikati na vilevile kunyunyiziwa maji.** Funika sasa kwa viungo vilivyosalia. Tabaka za awali hazitaonekana. Rudia utaratibu huu baada ya wiki tatu au kulingana na muda unaochukua viungo kuoza. Mboji yaweza kuwa tayari baada ya miezi 3.

Mkojo (fifisha kwa sehemu 4 za maji) waweza kunyunyiziwa ili kuharakisha kuoza. Mkojo pia huongeza viungo maalum kwenye mboji. Kiasi kidogo cha majivu laweza pia kunyunyiziwa.

Mkojo au majivu kupita kiasi hudhuru vimelea na vijidudu kwenye mboji.



Mfumo wa Indore: Kunyunyiza mkojo uliofifishwa kabla ya kufunika boji

Faida: Mfumo wa Indore huchukua muda mfupi kufanyiza mboji na ni rahisi kutunza. Mbegu za kwekwe na magonjwa huangamizwa.

Upungufu: Mfumo wa Indore huhitaji maji mengi na kazi nyingi. Mfumo huu hufaa iwapo una viungo vinavyohitajika kwa wingi.

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Kubadili mfumo wa Indore

Mfumo wa Indore waweza kubadilishwa kulingana na aina ya viungo vinavyoweza kupatikana. Iwapo kuna aina moja ya viungo kwa wingi, basi mfumo huu waweza kutumiwa kama ifuatavyo.

Sehemu za mvua chache

Katika sehemu kame, viungo vya mimea au samadi vyaweza kutayarishwa kama ifuatavyo:

1. Sentimita 15 ya majani na vijiti
2. Sentimita 30 ya majani yaliyotawanywa (hasa yale yaliyo na maji mengi)
3. Sentimita 30 za samadi au kinyesi
4. Sentimita mbili 2cm ya udongo wa juu ili kupata vijidudu na vimelea.

Rudia mpangilio huu hadi kufikia kimo cha urefu wa mita 1.5 juu. Funika kwa udongo, samadi au matawi ya migomba kuzuia unyevu kupotea.

Sehemu zilizo na mifugo wengi

Katika sehemu zilizo na mifugo wengi, utaratibu ufuatao waweza kuzingatiwa ili kutumia samadi. Mboji yapaswa kutengenezwa karibu na mahali pa malisho au zizi. Tayarisha kama ifuatavyo:

1. Sentimita 15 ya maganda makavu kama yale ya mahindi.
2. Ongeza tabaka ndogo za samadi kiasi cha sentimita 80 kila unapokusanya samadi.
3. Sentimita mbili za udongo wa juu.
4. Funika kwa tope, udongo au samadi.

Mfumo wa Bangalore

Mfumo wa Bangalore ni maarufu sana katika kutayarisha mboji. Baada ya kuweka viungo vifaavyo pamoja, mkusanyiko huu hufunikwa kwa matope na nyasi ili kuzuia hewa. Hii husababisha vijidudu visivyohitaji hewa (*anaerobic*) kusaidia mboji kuoza. Mboji hii yaweza kuwa na kimo cha mita moja m hadi 1.5 juu, upana wa mita moja na urefu wa mita 3. Mboji hii yaweza kuandaliwa kama ifuatavyo:

1. Tabakaya sentimita 10 (mabaki ya mazao kama vile mahindi). Nyunyizia maji.
2. Sentimita 10 ya viungo vinavyooza kwa urahisi (matunda na majani)
3. Sentimita mbili ya tabaka la samadi (Iwapo utapata)
4. Tabaka nyembamba ya udongo wa juu ili kutoa vijidudu na vimelea.
5. Rudia utaratibu wa safu hizi hadi kufikia mita moja hadi mita 1.5 juu.
6. Funika kwa matope udongotepetepe au nyasi zilizolowekwa.



Kufunika mboji kwa matope ili kuzuia hewa

Faida: Mfumo wa Bangalore huhitaji kiwango kidogo cha maji na hauna kazi nyingi kama kupindua mara kwa mara.

Upungufu: Mbegu za kwekwe na magonjwa yaweza kuhimili kiasi cha joto kwenye mboji hii. Sio rahisi kufahamu muda utakaochukua kwa mboji kuoza. Mfumo huu huhitaji maarifa katika shughuli ya utayarishaji.

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Mfumo wa Hamaki/ Ayari

Mfumo huu ni sawa na aina nyingine ya kutayarisha mboji ukizingatia matabaka. Hata hivyo matabaka ya mfumo huu hufata mpangilio fulani na huweza kutayarisha kiwango kikubwa cha mboji.

Joto hutolewa kila mara unapoweka ayari. Kila mara ayari hutengenezwa na kupangiliwa.

Kila ayari lapaswa kutengenezwa kwa upana wa mita mojahadi mita 1.5 kwa mita moja (usizidishe mita 3 kwa mita 3) na kimo cha urefu wa mita moja.

Siku ya kwanza ayari au faruma hutengenezwa kwa kukusanya viungo vya kutayarisha mboji. Baada ya siku mbili, hewa hulazimishwa kutoka kwa ayari kwa kukanyaga. Mfumo huu ni sawa na ule wa Bangalore, kwani mboji hukosa hewa na huwezesha vijidudu wasiohitaji hewa kutayarisha mboji.

Kati ya siku ya pili na tatu, ayari mpya hutengenezwa karibu na ile ya kwanza. Siku ya nne, ayari nyingine hutengenezwa juu ya ile ya kwanza, na kuzuia hewa kuifikia.

Utaratibu huu utaendelezwa hadi pale kila ayari kati ya hizo tatu ina ayari nyingine juu yake. Siku ya saba, ayari nyingine huandaliwa karibu na ile ya kwanza, na kurudia utaratibu huu. Picha inayofuata itakuelekeza katika kufahamu.

Faida: Mfumo huu hufaa katika kutayarisha mboji kwa kiwango kikubwa. Aidha mboji huendelezwa kwa muda mrefu.

Upungufu: Mfumo wa ayari hufaa tuu viwango vikubwa. Mfumo huu huhitaji kazi nyingi na viungo vingi. Mbegu za kwekwe na hata magonjwa hudumishwa kwa sababu ya kiwango kidogo cha joto. Ni vigumu kutazama jinsi mboji linavyooza. Mfumo huu huhitaji ujuzi na maarifa.




Siku ya 1: Tayarisha ayari ya 1



Siku ya 2: Tayarisha ayari ya 2




Siku ya 3: Tayarisha ayari ya 3 na kufinya ile ya 1




Siku ya 4: Tengenza ayari ya 4 juu ya ile ya 1 na kufinya ile ya 2



Siku ya 5: Tengeneza ayari ya 5 juu ya ile ya pili na kufinya ile ya 3



Siku ya 6: Tengeneza ayari ya 6 juu ya ile ya 3



Siku ya 7: Tayarisha ayari ya 7 karibu na ile ya 1, na kurudia utaratibu huu

Mfumo wa hamaki/ ayari


Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Mfumo wa joto jingi kutoka China


Mfumo huu umezingatiwa kwa miaka mingi kule China. Mfumo huu waweza kutumia aina nyingi ya viungo. Mfumo huu hufaa hata iwapo matumizi ni ya kinyesi cha binadamu, kiasi cha joto kwenye mfumo huu hufikia nyuzi joto 70 Celcius, hivyo basi kua viini vya magonjwa. **Ujuzi au utaalumu wahitajika kwasababu ya hatari ya magonjwa usipotunza vyema.**

Mboji hii ini upana wa mita 2 hadi 3 na urefu wa mita 6 hadi 7na kimo cha mita 1 hadi 1.5 kuelekea juu. Matayarisho ni kama yafuatayo:


1. Tengeneza tabaka la sentimita 15 hadi 30 la mabaki ya mimea.
2. Weka fito za mianzi zenye ukubwa wa kadiri ya sentimita 8 hadi 10 kipenyo mita mbili kila upande wa tabaka kwanza. Fito nyingine za mianzi zitapangwa ili kupitisha hewa.
3. Ongeza viungo vingine kwenye tabaka, kwa mfano majani, matawi, samadi na kinyesi, kufikia kimo cha mita 1.5.
4. Funika kwa udongo au tope lililo na majivu, mnanaa au machujo ya mpunga au ngano. Pande zapaswa kuegemea ili kushikilia udongo
5. Baada ya masaa 24 mkusanyiko hupata joto. Fito za mwanzo hutolewa ili kupisha hewa.
6. Mboji inapofikia kiasi cha nyuzi joto 60 hadi 70 celcius baada ya siku 4 au 5 mashimo huzibwa. Hii huzuia joto kupotea au unyevu kupita wakati wa msimu wa kiangazi au msimu wa masika.
7. Pindua mchanganyiko huu baada ya siku 14. Iwapo mchanganyiko umekauka, utahitajika kuongeza maji. Tayarisha na kufunika kwa udongo au tope jingine. Mboji litakuwa tayari baada ya wiki 8.



1. Tayarisha safu na fito za mwanzi



2. Jenga kando ya fito



3. Funika kwa udongo au tope



4. Toa zile fito za mwanzi

Mfumo wa China

Faida: Kinyesi cha binadamu hutumiwa kwa njia isiyo na madhara.

Upungufu: Mfumo huu huhitaji viungo vingi. Ni bora kufahamu mtindo huu bora zaidi kabla ya kuutekeleza.

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Mboji ya shimo

Mfumo huu hutumia mashimo yaliyochimbwa chini ya ardhi. Kina cha shimo hutegemea aina ya udongo na eneo la maji. Shimo la kawaida ni upana wa mita 1.5 hadi 2, na kina cha kuanzia sentimita 50 mpaka kina chochote. Waweza kutengeneza kuta za shimo kwa tope ili kuzuia maji kupotea. Kwa kawaida vijitaro au mashimo huchimbwa karibu karibu ili kurahisisha kazi ya kupindua. Tahadhari ili usichimbe karibu sana kiasi cha kuta kushikana.


Viungo vya kutengeneza mboji vitawekwa kwenye tabaka kama ilivyoelezwa hapa chini. Iwapo shimo ni kubwa kama upana wa mita 2, urefu wa mita moja, basi tumia lita 1 hadi 1.5 za maji kabla ya kufunika shimo kwa udongo.

Tabaka zichukue utaratibu ufuatao:

1. sentimita 10 ya viungo visivyooza kwa urahisi (mabaki ya mimea kama mahindi)
2. Sentimita 10 ya viungo vinavyooza kwa urahisi (matunda na mboga)
3. sentimita 2 ya samadi (iwapo utapata)
4. Kiasi kidogo cha udongo wa juu ili kupata vijidudu na vimelea kusaidia katika kazi ya kuoza.
5. Rudia utaratibu huu hadi mboji kufikia kimo cha mita 1 hadi 1.5 juu.
6. Funika kwa nyasi au matawi (kama yale ya migomba) ili kupunguza kupotea kwa maji.

Baada ya wiki 2 hadi 3, mchanganyiko katika shimo hili upinduliwe na kutiwa kwenye shimo la pili, kisha pia baada ya wiki zingine 2 hadi tatu kubadilishwa kwenye shimo la 3. Unapotoa viungo kwenye shimo la kwanza, tayarisha viungo vingine na kujaza shimo hilo upya. Endeleza utaratibu huo kufanya mzunguko wa kutayarisha mboji.

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II



Faida: Mfumo huu ni mwepesi na hutengeneza mboji kwa haraka. Aidha mfumo huu hautahitaji fedha wala gharama nyinginezo. Mfumo huu hauhitaji maji mengi hivyo basi hufaa hata sehemu kame.

Upungufu: Ni vigumu kufuatiliza utaratibu wa kasi ya kuoza ukilinganisha na mifumo ya hapo awali. Ni kazi nyingi kuchimba mashimo.

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Mboji ya mtaro


Mfumo wa mboji ya mtaro ni kama ule wa shimo, ila tu mimea hupandwa kwenye mitaro bila kupindua na kugeuza mboji. Tayarisha mtaro kabla ya kupanda. Kiasi cha mtaro hutegemea aina ya viungo vilivyoko na aina ya mimea unayotarajia kupanda. Upana waweza kuwa sentimita 50 hadi kiwango chochote kile, kina chaweza kuwa mita 1 au chini ya mita moja. Funika mtaro ukizingatia maelezo yafuatayo:

1. sentimita 10 ya viungo visivyooza kwa urahisi (mabaki ya mimea kama mahindi)
2. Sentimita 10 ya viungo vinavyooza kwa urahisi (matunda na mboga)
3. Sentimita mbili ya samadi (iwapo utapata)
4. Kiasi kidogo cha udongo wa juu ili kupata vijidudu na vimelea kusaidia katika kazi ya kuoza.
5. Rudia utaratibu huu hadi mboji kufikia sentimita 50 juu.
6. Funika kwa nyasi au matawi (kama yale ya migomba) ili kupunguza kupotea kwa maji na kuacha kwa muda wa mwezi mmoja kabla ya kupanda.

Hautahitajika kulima sana iwapo utazingatia mfumo huu jinsi ulivyo kwenye picha. Lazima kuacha sehemu hiyo kwa mwezi mmoja ili viungo vioze. Iwapo sehemu ya mitaro ni pana, basi waweza kupanda mimea mingi kwenye eneo hilo.

Faida: Mfumo huu hufaa sana hasa katika sehemu zilizo na mchwa.

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II



Vijitaro vilivyojazwa viungo vy kutengeneza boji


Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Mboji ya Kikapu

Iwapo hauna viungo vingi vya kutengeneza mboji, basi waweza kutumia mfumo huu. Mfumo huu hufaa bustani ya nyumbani mahali pa kukuza mboga. Mtindo huu ni kama ufuatao:

1. Chimba shimo la duara lenye kipenyo cha sentimita 60 na kina sentimita 60
2. Jaza chini viungo visivyooza kwa urahisi (vijiti na mabua)
3. Ongeza tabaka la samadi kina sentimita 8
4. Ongeza tabaka la sentimita 15 la majani (matawi yaliyo mabichi)
5. Ongeza majivu sentimita 0.5
6. Rudia utaratibu wa 3 hadi 5 mpaka kujaza shimo
7. Funika kwa nyasi au matawi ili kuzuia unyevu kupotea
8. Kwa kutumia fito nyembamba zungusha ili kutengeneza kapu la hadi sentimita 10juu ya ardhi

Waweza kupanda mbegu au miche kwenye kapu hilo. Mimea itatumia rutuba itokanayo na mboji hii.



Miche kwenye 'kapu'

Ni bora kutengeneza vikapu kwenye sehemu mbali mbali katika bustani ili kuimarisha rutuba.


Faida: Mboji ya kikapu hutumia masalio ya jikoni na ni rahisi tengeneza.

Mboji ya Boma

Mfumo huu hufaa katika kilimo kinachohusisha mifugo (Ng'ombe, kondoo, mbuzi, sungura na kuku), Kinyesi cha mifugo ndicho kiungo maalum pamoja na mabaki ya vyakula.

Kinyesi na mkojo huchangia sana katika kuimarisha rutuba. Ni bora pia kubadilisha matandiko ya mifugo kila baada ya wiki moja. Iwapo utatumia matandiko kama mabaki ya mimea, machujo ya mbao, matawi na kwekwe, basi viungo huongezeka kila mara.

Ni bora kuepusha mvua au maji dhidi ya kusomba viungo hivi.



Zizi lililoezekwa na kutiwa matandiko


Viungo hivi vyaweza kukusanywa kila siku au hata kabla ya wiki moja. Iwapo ni kila siku viungo vyapaswa kufunikiwa mahali ili visikauke na kupoteza nguvu.

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Fuata utaratibu ufuatao:

1. Chimba mitaro 3, kina cha sentimita 30, karibu na boma au zizi la mifugo ili kurahisisha usafirishaji.
2. Weka majani makavu chini ya vijitaro hivyo.
3. Ongeza sentimita 10 ya samadi pamoja na matandiko kutoka kwa boma.
4. Ongeza sentimita 5 ya udongo wa juu ili kupata vijidudu na vimelea kutekeleza kazi ya kuoza.
5. Ongeza sentimita 10 ya samadi au matandiko kutoka kwa boma hilo.
6. Endeleza utaratibu huu hadi kufikia mita 1 mpaka 1.5 juu. Wakati wa kiangazi tengeneza hadi mita 1.5. Wakati wa mvua fikisha mita 1 ili kuzuia maji kusomba mboji.
7. Funika kwa nyasi, mabaki ya mimea au matawi ya migomba kuzuia ukavu au maji kupita kiasi.

Badilisha na kupindua viungo vilivyo kwenye mtaro wa kwanza na kuhamishia ule wa pili baada ya wiki 2 au 3, kisha kutoka ule wa pili hadi wa tatu baada ya wiki 2 hadi 3. Funika mboji iwapo hautatumia moja kwa moja. Funika kwa matawi ya migombai nyasi, au hata udongo.



Geuza viungo na kuhamisha ha kwenye vijitaro ili kutengeneza boji

Kutayarisha mboji kwa kutumia aina mbali mbali ya viungo

Matumizi ya viungo mbalimbali kutayarisha mboji hutoa mboji ya hali ya juu. Kwa wakati fulani waweza kuwa na aina moja ya viungo kupita kiasi. Waweza kukosa viungo vingine vya kuongeza, lakini waweza kutoa mboji la hali ya juu.

Matumizi ya mabaki ya nyumbani

Mabaki ya nyumbani hujumuisha mabaki kutoka jikoni, uchafu wa kufagiliwa, makaratasi au majivu. Usitumie plastiki au chupa na mikebe. Halikadhalika usitumie mabaki kutoka machinjioni au nyama kwani utavutia wadudu wanaosababisha magonjwa na harufu mbaya. Aidha pia usitumie kinyesi cha binadamu, mbwa au paka. Ni bora pia kuwa na uangalifu na kuzuia kutumia aina moja ya kiungo.

Baadhi ya mabaki haya hutolewa kwa viwango vidogo mara kwa mara. Ni muhimu kukusanya kiasi kingi kisha kumwaga kwenye mboji kufikia safu ya sentimita 30. Mabaki haya huhitaji hewa nyingi ili kutengeneza mboji.

Matumizi ya gugu-maji

Gugu-maji hujumuisha madini mengi yaliyo na umuhimu katika kuimarisha rutuba. Kwa wale wakulima walio karibu na ziwa au bahari waweza kupata viungo hivi. Iwapo gugu-maji lina kiasi kingi cha chumvi, ni bora kuivunja chumvi hii. Gugu-maji lililo kaushwa hupoteza kiasi cha chumvi. Tumia kwa pamoja na viungo vingine. Ni rahisi sana kutayarisha mboji kutoka kwa gugu-maji. Njia nyingine ni kukausha na kuponda kisha kunyunyiza viungo hivi kando ya mimea.

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Machujo ya kahawa


Katika sehemu za viwanda au kinu cha kahawa machujo hupatikana kwa wingi. Sehemu hizi hutoa harufu mbaya na kuzalisha wadudu.

Machujo ya kahawa yanayo madini mengi yanayofaa katika kutengeneza mboji kwa mfano, *nitrogen* na *potassium*. Ni bora kutayarisha viungo hivi wala sio kumwaga kwenye shamba.

Viungo hivi huhitaji hewa, ni bora kuweka kwenye visanduku vilivyoinuliwa au sehemu iliyoinuliwa hadi kufikia mita 1. Sehemu hii yapaswa kuezekwa ili maji ya mvua yasifagie viungo hivi. Muinuko huu waweza kutengenezwa na mianzi iliyoinuliwa kwa tofali au mawe.

Kabla ya kutayarisha mboji, toa majimaji kwenye machujo hayo. Waweza pia kuongeza viungo vingine kama mabaki ya mboga kisha kuongeza udongo kidogo.

Geuza mboji kila baada ya wiki 4 au 6, mboji litakuwa tayari baada ya miezi 4 hadi 6.



Sehemu iliyo nuliwa kwa kutengeneza a boji kutoka kwa machujo ya kahawa

Kutayarisha mboji ukitumia mimea ya maji

Mimea inayopatikana kwenye maji (kama gugu) husababisha shida kwa shughuli ya uvuvi au usafiri wa maji. Kuangamiza gugu kwa matumizi ya kemikali ni hatari kwa mazingira. Halikadhalika ni ghali na hupoteza wakati! Gugu na mimea mingine yaweza kuwa na faida iwapo utatayarisha na kutumia kama ifuatavyo:

1. Ng'oa gugu na mimea mingine kutoka kwenye maji kisha kukausha.
2. Mboji yaweza kutengenezwa ukijumuisha viungo hivi pamoja na jivu, udongo, samadi na mabaki kutoka jikoni. Zingatia mfumo wa Indore katika kutengeneza matabaka.

Mboji iliyotengenezwa kwa kutumia gugu-maji bila kuongeza viungo vingine halitafaa sana, hivyo basi tumia kwa kiwango kidogo.

Kutayarisha mboji ukitumia kinyesi au taka-maji

Kuna hatari nyingi katika kutumia taka-maji au kinyesi cha binadamu kwa kutayarisha mboji. Magonjwa yaweza kusambazwa kwa urahisi kupitia kwa viungo hivi. **Lazima kutahadhari, ni bora pia kuwa na maarifa au ujuzi wa kutumia viungo hivi.** Mfumo wa China ndio hufaa katika kutayarisha mboji kwa kutumia viungo hivi. Mfumo huu huangamiza wadudu na viini vya magonjwa. Lazima kiwango cha joto kiwe cha juu kuwa viungo hivi. Hata hivyo, maelezo haya sio kikwazo katika matumizi ya kinyesi cha binadamu na taka-maji kutengeneza mbolea, bali wapaswa kuwa na uangalifu.

Kutayarisha mbolea ya mboji katika nchi za hari II

Marejeleo

'The Preparation and Use of Compost; Agrodok 8' (1990) by Inckel, M. et al AGROMISA, PMB 41, 6700 AA, Wageningen, The Netherlands

'Field Notes on Organic Farming' (1992) Njoroge, J. Kenya Institute of Organic Farming, PO Box 34972 Nairobi, Kenya

Majulisho

Maelezo ya ziada kuhusu; Viunga vya miche, Mboji ya Kijani, Kuzuia kwekwe, Miti yenye manufaa kama vile Mwarobaini na Mzunze, Kilimo Hai, na jinsi ya kukabili Magonjwa na wadudu yanaweza kupatikana kutoka HDRA:

The Organic Advisory Service
HDRA – International Development Programme
Ryton Organic Gardens
Coventry CV8 3LG
UK

Simu: +44 (0)24 7630 3517

Kipepesi: +44 (0)24 76623 9229

Barua-pepe: ove-enquiry@hdra.org.uk

Mtandao: www.gardenorganic.org.uk/international_programme/

Madhumuni ya shirika la HDRA ni kufanya utafiti, kutoa na kueneza habari kuhusu Kilimo Hai, Ukulima na chakula katika Uingereza (UK) na Dunia nzima. Mwongo mmoja uliopita, shirika hili limekuwa likisaidia katika kubuni njia za kuboresha na kutafiti aina ya ukulima hasa Kilimo Hai katika nchi za hari (Tropics). Vilevile kutoa maelezo na majarida kuhusu Kilimo Hai na pia kutoa mbegu na maelezo ya upanzi.

Maelezo haya yanaweza kunakiliwa bure kwa njia yoyote pasipo malipo.

Tafsiri na:

Patrick Bunyali Kamoyani, P.O Box 1, 50321-Magada via Maragoli, Kenya.
pbkamoyani@excite.com

Kimehaririwa na Leonard Mtama

